**Deutsche Welle Radio**
**“Learning By Ear”**
**Elimu na mafunzo 1:MUUGUZI**

**MWANDISHI : Richard Lough, Kenya**
**WAHARIRI : Ulrich Neumann, Maja Dreyer**
**TAFSIRI : ERIC PONDA**

**1 Msimulizi**
**1 Sauti : Judith (miaka 29)**

**Intro**

Hujambo na karibu kwa makala haya ya “Learning by Ear” Noa bongo jenga maisha yako, vipindi vinavyozungumzia zaidi masuala ya mafunzo na Kazi.Katika mfululizo wa vipindi 8 vijavyo tutawajulisha kwa watu wa taaluma mbali mbali wakizungumzia taaluma zao *(na Ikiwezekana pia kugusia au kukushauri jinsi unavyoweza kujiunga na sekta au taaluma hizo)*

Katika makala yetu ya leo tunakutana na Judith, msichana anayefanya kazi ya Uuguzi katika Hospitali moja ya kitaifa nchini Kenya.

**1. SFX_WODI**

**2. O-Ton Judith_1**

Naitwa Judith Mweu. Nafanya kazi katika hospitali ya kitaifa ya Kenyatta, katika wodi maalum itwayo 10c, ambako hupokea wagonjwa wa aina mbalimbali. Katika wodi huwapokea na kuwahudumia wagonjwa wanaohitaji upasuaji, au wanaohitaji kuwa chini ya uchunguzi maalum. Katika kitengo au wodi hii, sisi hufanya uchunguzi na utafiti wa kina kubainisha ugonjwa halisi na sio tu kutibu ugonjwa tusioujua chanzo chake.

**3. SFX: X-fade into SFX_ Sauti ya vitu vikipangwa -madawa, sindano…na TROLI likisukumwa.**

Judith Mweu mwenye umri wa miaka 29 sasa anajiandaa kwa zamu ya mchana katika Hospitali kuu ya kitaifa iliyoko mji mkuu wa Nairobi nchini Kenya.

Judith alifuzu kwa kazi hii ya uuguzi miaka sita iliyopita. Baada ya kukamilisha mafunzo yake ya uuguzi, alifanza mazoezi ya utenda kazi katika Hopsitali tatu tofauti nchini humo. Alimaliza mafunzo hayo ya utenda kazi wa 2003 na kujiunga na Hospita hii ya Kenyatta mwaka mmoja baadaye.

Ni muda mfupi baada ya saa sita za mchana na Judith tayari ameanza kupanga vitu atakavyotumia baadaye kwenye troli, glavu, sindano na madawa na kuanza safari ya kulikokota troli hilo hadi Wodi.

**4. O-Ton Judith_2**

Hapa tuko na jumla ya vitanda 23. Leo tuna vitanda 3 ambavyo ni vitupu havina wagonjwa. Lakini wakati mwengine, hasa wakati ule wa ghasia za baada ya uchaguzi, wodi ilikuwa imejaa..

**1. SFX_Ward [runs underneath throughout]**

Hospitali kuu ya Kenyatta ndiyo Hopsitali kubwa zaidi ya umma inayofadhiliwa na serikali nchini Kenya. Inajumla ya vitanda 2000 anasema Judith. Hospitali hii imewaajri maelfu ya wauguzi, madakatri wakiwemo wale wa upasuaji vile vile washauri. Wafanyi kazi hawa hufanya kazi usiku na mchana kwa zamu, ingawa utaratibu huo unategemea ratiba ya zamu. Na hapa Judith anatueleze kazi atakayoifanya hivi leo.

**5. O-Ton Judith_3**

Kwa kawaida shughuli zangu hapa ni kuwapa wagonjwa madawa. Tuna aina mbili za madawa, tembe na sindano. Mbali na hayo huwasaidia wagonjwa ambao hawawezi hata kujigeuza kitandani na pia kujaribu kuwapa imani na matumaini. Huwa tunawapa ushauri, kuwachunguza hasa mpigo wa moyo, kiwango cha sukari na shinikizo la damu mwilini.

**6. SFX_Judith_Patient_1 [full up for 10 seconds then fade down and under next track]**

Mgonjwa wa kwanza kuonekana na Judith ni Anya Wambui. Anya anakabiliwa na ugonjwa wa Sukari, na hali yake imezidi katika siku chache zilizopita. Sasa hawezi hata kuzungumza vizuri. Judith anamuliza anavyojisikia na kisha kuanza kumpima mpigo na shinikizo la damu mwilini.

**6. SFX_Judith_mgonjwa _1 [Sauti yapandishwa kuanyizia `Ok, hebu tupime kiwango cha msukumo wako wa damu`, hadi shughuli ya kumpima mgonjwa inapokamilika.**

Akiwa amekalia kitanda cha mgonjwa huyo, Judith anaonyesha wingi wa huruma na mapenzi: Kwa unyenyekevu anazungumza na kumueleza kila mgonjwa anachofanya na sababu za kufanya hivyo. Judith anasema tayari wagonjwa hao wanakabiliwa na dhiki na wanahitaji mapenzi. Anasema kuwa yeye na wauguzi wengine hujaribu kuwapa mapenzi wagonjwa ili kuowapunguzia dhiki hizo.Huku akitizama ripoti ya Daktari, Judith anaeleza anachotafuta…..

**7. O-Ton Judith_4**

Huwa tunamchunguza mgonjwa kwa ujumla. Nikimtizama nataka kusikia sauti yake, ili kesho nikirudi niweze kujua kwa urahisi mgonjwa anavyoendelea. Ni rahisi kujua na kuelezea mabadiliko hayo. Kwa mfano leo anapoteza sauti, lazima kuna mabadiliko…. Kwa hiyo kila ninapokutana na mgonjwa kwa mara ya kwanza, ni lazima nijue hali yake halisi na kisha, kuanzia hapo nitaweza kujua kwa haraka mabadiliko au jinsi mgonjwa huyo anavyoendelea. Hivyo hatua za haraka zinaweza kuchukuliwa mgonjwa anapozidiwa au mambo yanapokwenda mrama.

Tangu utotoni Judith alitaka sana kuwa muuguzi. Anasema kuwa alikuwa akitembelea sana hospitali ya kijijini mwaka anapougua kidogo. Na kila mara alipotembelea Hospitali hiyo, alifurahishwa sana na kazi za Madaktari na wauguzi. Hivyo alipokuwa shuleni pia alitaka kuwa Daktari au muuguzi. Alifahamu kwamba hiyo ndiyo taaluma angependa kufanya kutibu na kuuguza wagonjwa na jamaa zake.

Lakini anaushauri kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na taaluma hii. Digrii ya uuguzi ni ngumu na inahitaji uwe umepita vizuri shuleni!. .

**8. O-Ton Judith_5**

Ni kazi ngumu. Wakati wa kusomea kozi hiyo, utatambua ni kwa nini wanataka uwe umepita vizuri shuleni…. Kwani kozi hii inahitaji mtu aliyejitolea, kutokana na kazi nyingi. Darasani tulikuwa jumla ya wanafunzi 69, lakini ni wanafunzi 25 pekee waliomaliza na kufuzu kozi hiyo… Kwa hiyo, hii inaonyesha wazi kwamba si taaluma rahisi. Mafunzo ya uuguzi kama mafunzo mengine ya sayansi ya afya, taaluma hii inahitaji mtu awe na umakini. Na hii ndio maana wakufunzi huwa wakali kuliko wale wa kozi nyingine.

Lakini ningependa pia kuwahimiza wale wanaotaka kusomea taaluma hii anasema Judith. Kwani huwa na matunda mazuri pale Mtu anapofuzu katika taaluma hii.
Hakuna kitu kizuri cha kufurahisha kama kumuona Mgonjwa akiondoka kitanda cha Hospitalini na kurudi nyumbani baada ya kupata nafuu kutokana na huduma zako.

**9. SFX_Mgonjwa _2**

Judith anasonga hadi kitande kingine na ambapo anatuhusia kwamba kazi hii inahitaji ustahimilivu. Katika Hospitali yoyote kifo huwa kiko machoni tu, maana watu wanafariki kila dakika na ni lazima uzoee hali hiyo. …

**10. O-Ton Judith_6**

Mara nyingine inavunja moyo kwa sababu mara juhudi zetu kuwahudumia wagonjwa huambulia patupu pale mgonjwa anapofariki. Wagongwa huwa na matatizo tofauti na jinsi anavyoitikia matibabu. Wengine huitikia vyema na ikawa ngumu kwa wengine… Kwa hivyo baada ya kujitahidi kumhudumia mgonjwa kadri ya uwezo wako na mwishowe usifaulu, kwa kweli inavunja moyo..

**11. SFX_Mkahawani**

Ni wakati wa punga hewa kidogo na Judith anakwenda katika mkahawa wa ndani Hospitalini humo. Mara nyingi huwa na kazi ngumu na inahitaji makini, anasema Judith. Ukifanya makosa kidogo tu unaweza hata kumuua mgonjwa, anaongeza huku akinya Soda na kuwaza jinsi ya kuboresha utendaji kazi wake.

**12. O-Ton Judith_7**

Muuguzi mzuri lazima awe mstahamilivu na kuwaelewa wagonjwa na jamaa za wagonjwa hao. Kwa sababu unapokuwa unamhudumia mgonjwa wako, huwezi kuepukana na jamaa zake.

Ni dhahiri kwamba Judith ameonyesha ustahamilivu mkubwa na mwenye kuifahamu vyema kazi yake.
Jambo linalo msikitisha zaidi ni idadi ya madaktari na wauguzi kutoka nchini humo wanaohamia mataifa ya bara ulaya na Marekani kutafuta pato zuri. Judith anakiri kwamba uhamiaji wa watu wenye ujuzi kutoka Africa kumathari pakubwa kiwango cha utoaji huduma hasa katika sekta ya sekta ya afya

**13. O-Ton Judith_8**

Ni wengi sana wanaohamia mataifa ya Ulaya. Hali hii inaathiri sana sekta ya afya barani Afrika. Kwa sababu Marekani na Uingereza ni nchi zilizostawi, na madaktari wengi na wauguzi huhamia nchi hizi kutafuta mishahara mizuri na mazingira mazuri ya kufanya kazi.

**14. SFX_troli na mazingira ya Wodi**

Judith anakiri kwamba watu wengi hushawishika kwenda kufanya kazi nchini Uingereza. Na anaporejea kazini kwa awamu ya pili katika wodi hiyo ya 10c, Judith anasisitiza kwamba anataka kubakianchini Kenya kuendelea kuwasaidia Wakenya. Kwa wale wanaotaka kufuata nyayo zake, hapa Judith anaushauri.

**15. O-Ton “Ushauri wa ” Judith**

Ningependa kuwashauri na kuwahimiza wale wote wanaotaka kusomea taaluma hii, kwamba ni taaluma nzuri, lakini ni sharti wajifunge kibwebwe kukabiliana na changamoto kama vile kusoma kwa bidii na

kuyachukulia mikononi maisha ya wengine. Lazima uwe muangalifu, hilo ni sharti moja wapo..! Na mwishowe changamoto hizi huwa za manufaa makubwa pale unapoona juhudi zako zikiokoa maisha ya wengine.

Baada ya mampumziko hayo. Judith amerejea kwa awamu ya pili kazi katika wodi 10c. Hapa huwa na shughuli nyingi anasema Judith, na huwezi kujua nini kitakachotokea baadaye.

**Outro**

Na kutoka Hospitali kuu ya Kenyatta mjini Nairobi Kenya, umesikia jinsi Judith ambaye ni muuguzi katika hospitali hiyo alivyofikia uamuzi wa kujifunza taaluma ya uuguzi.– kazi ngumu nzuri ingawa yenye changamoto nyingi kama asemavyo, Na hadi kufikia hapo hatuna budi kuwaageni kwa kipindi cha leo cha "Learning by Ear" kuhusu ajira.Iwapo unataka kujifunza mengi zaidi kuhusu vipindi hivi vya "Learning by Ear", au kusikiliza tena makala haya tutembelee katika mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.